TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION (TARO)
(TAASISI YA HAKI ZA WASANII)
S.L.P 70624 Dar es salaam, Simu:+255785769223,+255767292581
Barua pepe:tarotanzania@gmail.com,Mitandao ya kijamiii:instagram/fb, taro.tz
Anwani ya Ofisi: Mtaa wa Kihonzile , Mkabala na Daraja la kuelekea Bagamoyo, Kata ya Mabwepande , Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam
"Tunasimama kwa ajili ya Haki na Maslahi ya wasanii wote"

Kumb na: Taro /P/2022/ A17 **: Swahili Version:** Tarehe: 26 Julai 2022

# "MAPENDEKEZO YA TARO KWA KAMATI YA KUSIMAMIA HAKIMILIKI"

## CMO ZAGEUZWA LEBO YA MUZIKI NA SHERIA MPYA YA FEDHA NAMBA 5 YA MWAKA 2022 (ILIYOANZA KUTEKELEZWA TAREHE 30 MWEZI JUNI 2022

Rejea kichwa cha habari hapo juu. **Tanzania Artists Rights Organization (TARO)** au kwa lugha ya Kiswahili **"TAASISI YA HAKI ZA WASANII"** ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiliwa kushughulikia haki na maslahi ya wasanii wote Tanzania.

Mnano tarehe **16 Mwezi Juni 2022**, serikali iliwasilisha bungeni mswaada wa **Sheria ya Fedha ya mwaka 2022**. Katika mswaada huo kulijumuisha mabadiliko ya baadhi ya vifungu vya sheria ya hakimiliki na haki shirikishi iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002)**. Mswaada huo ulipitishwa na bunge kuwa sheria yaani **(Sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022).** Sheria hiyo ilianza kutumika mnamo tarehe **30 Mwezi Juni 2022**.

Mnamo tarehe **19 Mwezi Julai 2022**, kamati ya kuratibu ukusanyaji wa maoni ya namna bora ya kusimamia hakimiliki nchini ilianza kukusanya maoni.

**TAFAKARI:** Je tunapitisha sheria kwanza kisha tunakusanya maoni kwa wadau au tunakusanya maoni kwanza ndio tunapitisha sheria?

**TARO** tunaipongeza **Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo** na iliyokuwa **Copyright Society of Tanzania (COSOTA)** ambayo kwasasa ni **Copyright Office of Tanzania (COOTA)** kupitia **Mh.Waziri (Mohamed Mchengerwa)** kwa kusikia na kutendea kazi changamoto mbalimbali zinazowakabili wabunifu nchini haswa haswa wasanii. Pia kwa niaba ya wasanii nchini, TARO tunaishukuru serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na **Mh. Raisi, Mama Samia Suluhu Hassan** kwa kuchukua hatua na kuanza kushughulikia changamoto za wasanii nchini. Tunaamini kwenye nia njema ya serikali.

**A.** YAFUATAYO NI MAPUNGUFU YA SHERIA YA FEDHA NAMBA 7 YA MWAKA 2022 ILIYOREKEBISHA SHERIA YA HAKIMILIKI NA HAKISHIRIKISHI - **COPYRIGHT AND NEIGHBOURING RIGHTS ACT. NO.7 OF 1999 (CAP.218.R.E. 2002)**

   i. **Sheria imeunda makampuni yanayofanyakazi zaidi ya kukusanya na kugawa mirabaha (yanayoweza kutumia haki zote zinazolindwa na hakimiliki katika kazi ya kibunifu sawa lebo ya muziki).**

Kwa mujibu wa kifungu cha **23** cha sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, kimebadili kifungu cha **4** cha Sheria ya Hakimiliki na Haki Shirikishi iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002)** kwa kuweka kipengele kinachoelezea maana ya **" kampuni ya kukusanya na kugawa mirabaha (CMO)".** Sheria inaelezea kuwa CMO ni shirika au bodi inayotumia hakimiliki au haki zinazohusiana na hakimiliki kwa niaba ya mmiliki wa hakimiliki, ambapo lengo lake kuu ni kujadiliana kuhusu kukusanya na kugawa mirabaha na kuruhusu matumizi ya kazi zinazolindwa na hakimiliki, pia kuruhusu kuchezwa kwa kazi ambapo, itakata ada kwa ajili ya kujiendesha.

Ukirejea maneno haya ***"…..the granting of licenses in respect of copyright works……."*** kwenye kifungu hicho, yanahalalisha CMO kujifanyia kazi nyingine zaidi ya kukusanya na kugawa mirabaha kwenye kazi zinazolindwa na hakimiliki . Kifungu hicho kimeweka mwanya wa matumizi mabaya ya ofisi ya umma (CMO) kwa maslahi binafsi.

Kwa mujibu wa kifungu cha **28** cha sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, kimeongeza kifungu kipya cha **52B** katika Sheria ya Hakimiliki na Haki Shirikishi iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002).** Katika kifungu hicho cha **52B** kwenye kifungu chake kidogo **(h)** kinaitambua CMO kama wakala wa wanachama wake wote kuhusiana na haki zote zinazolindwa na hakimiliki kwenye kazi zao za kibunifu.

Kifungu **52B(h)** cha sheria tajwa hapo juu kinaifanya CMO kuwa na mamlaka sawa na **lebo ya muziki** kwa msanii bila hata msanii kuingia mkataba wowote na CMO kwa lengo hilo. Pia kinazidi kukazia uhalali wa CMO kutumia kazi za wasanii zinazolindwa na hakimiliki kwa namna yoyote ile isipokuwa tu, kuamisha umiliki. CMO inaweza kuruhusu kuchapisha na kusambaza CD ya albamu ya muziki wa msanii, CMO inaweza ikachukua nyimbo za msanii na kuzisambaza mtandaoni bila ruhusa ya msanii husika. CMO inaweza kuingia mkataba wa kibiashara wowote kwenye kazi ya msanii bila ruhusa ya msanii. Ambapo jambo hilo sio lengo la wasanii kutaka kuwa na CMO.

**<u>Mapendekezo:</u>**

Sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, inapaswa kurekebishwa na kuweka wazi kuwa, CMO itakayopewa leseni ya kukusanya na kugawa mirabaha, itakuwa wakala kwa msanii kwa lengo la kukusanya na kugawa aina Fulani ya mirabaha tu na si vinginevyo, pia sheria ielezee wazi aina za mirabaha kutokana na aina za sanaa na mahali inapokusanywa. Mfano:Mirabaha ya Muziki kutoka sehemu zote za umma zinazotumia muziki(ziorodheshwe), Mirabaha ya kazi za fasihi kutoka sehemu zote za umma zinazotumia fasihi (ziorodheshwe). Pia sheria isiruhusu CMO kufanya shughuli nyingine zaidi ya kukusanya

mirabaha husika kwa mwanachama wake. Pia sheria ielekeze kuwa taarifa za mirabaha kutoka nje ya nchi lazima ziwekwe wazi kwenye umma muda mfupi baada ya kupokelewa. CMO zisifanye makato yoyote kwenye mirabaha kutoka nje kwasababu hazijaingia gharama yoyote kukusanya.

**ii. Sheria haijaweka wazi kutakua na aina ngapi za CMO na aina hizo zitapatikana kwa vigezo gani.**

Kwa mujibu wa kifungu cha **28** cha sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, kimeongeza kifungu kipya cha **52A** katika Sheria ya Hakimiliki na Haki Shirikishi iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002).** Katika kifungu hicho cha **52A** kifungu chake kidogo **(2)** kinakataza kuwa na CMO zaidi ya moja kukusanya na kugawa mirabaha kwenye ubunifu wa aina moja. Ingawa sheria haijaweka wazi kutakuwa na aina ngapi za CMO na hizo aina za CMO zinapatikana kwa vigezo gani. Pia sheria imeacha mwanya kwa kutojionya kuwa *taratibu za upatikanaji wa leseni kwa CMO zinapaswa kuwa za uwazi zenye kuzuia mazingira ya rushwa.*

<u>**Mapendekezo:**</u>

Sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, inapaswa kurekebishwa kuonyesha kutakuwa na aina ngapi za CMO na aina hizo zitapatikana kwa vigezo gani. Hili ni suala la kushirikisha wadau watoe maoni yao. Pia sheria inapaswa kuweka wazi mchakato mzima wa CMO kupata leseni, sheria inapaswa kuweka utaratibu unaoruhusu ushindani katika upatikanaji wa leseni kwa CMO. Hii itasaidia kuondoa mazingira ya rushwa katika upatikanaji wa leseni kwa CMO na kupata CMO zenye ufanisi. Kwa sheria hii iliyopo kuna mwanya mkubwa unaoruhusu mazingira ya rushwa katika upatikanaji wa leseni kwa CMO.

**iii. Kusajili CMO kupitia sheria ya Makampuni ya 2002 ni kutengeneza mkanganyiko wa hali ya juu na kutajirisha baadhi ya watu binafsi.**

Kwa mujibu wa kifungu cha **28** cha sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, kimeongeza kifungu kipya cha **52C** katika Sheria ya Hakimiliki na Haki Shirikishi iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002).** Katika kifungu hicho cha **52C** kifungu chake kidogo **(c)** kinaelekeza kuwa CMO lazima isajiliwe kama kampuni kwa kufuata sheria ya Makampuni ya 2002.

Ifahamike kuwa CMO ikisajiliwa kama kampuni, utaratibu wa kuwa mwanachama utaongozwa na **Sheria ya Makampuni ya 2002**. Wanachama lazima wawe wamiliki wa CMO kwa kufuata taratibu za sheria ya Makampuni. Wanachama wakizidi 50, CMO inabadilika na kuwa **kampuni ya umma** hata kama CMO ilisajiliwa kama Kampuni isiyotengeneza faida. Ifahamike kuna wabunifu zaidi ya 1000 nchini kwa hiyo tunategemea wanachama kuzidi 50 katika CMO. CMO ikibadilika kuwa **kampuni ya umma** lazima iendeshwe kama

biashara kwa mfumo wa kutengeneza faida na kila mwisho wa mwaka, itapaswa kugawa gawio la faida (dividend) kwa wanachama wake (wamiliki). Masuala ya kisheria tunayopaswa kujionya yameelezewa kama ifuatavyo:-

- Kuruhusu CMO kusajiliwa kama kampuni isiyotengeneza faida kwa sheria ya Makampuni ya 2002, kuna hatari ya kufanya **wanachama 30** wa mwanzo kuwa **matajiri sana** kwasababu, kwa uhalisia wanachama wabunifu ndani ya CMO lazima watazidi 50, pale CMO itakapoanza tu kufanya kazi, wakizidi 50, CMO itageuka kuwa **kampuni ya umma**, ambapo wale **wanachama 30** wa mwanzo watakua waamuzi wa kuu wa mwanzo katika kuunda **kampuni ya umma**. Wale **wanachama 30** watakapokua waamuzi wakuu wataweza kuamua kiasi gani cha hisa (umiliki wa CMO) kiwe kwa ajili ya umma na kiasi gani kibaki kama mali yao. Wanaweza wakatoa kiasi kidogo cha hisa kwa ajili ya umma na kiasi kingi wakajimilikisha wao. Ifahamike wakichukua kiasi kikubwa cha hisa (umiliki), pia watachukua kiasi kikubwa cha faida itakayopatikana kwenye kampuni ya CMO. Kwasababu sheria haijakataza CMO kutumia mirabaha kufanyia biashara, CMO inaweza kuchukua mirabaha ya wabunifu na kufanyia biashara, kisha faida ikagawanywa kulingana na umiliki wa hisa ndani ya CMO. Kama CMO itafanya biashara, basi inaweza ikatumia pesa za mirabaha kufanyia biashara na kujigawia faida, kisha baadae ikafanya makato kwenye hiyo mirabaha kwa ajili ya kujiendesha, alafu mirabaha itakayobaki ikagawanywa kwa wabunifu (wanachama). Je hili ndio lengo la CMO?
- CMO ikiwa **kampuni ya umma** wanachama wake wote watawajibika kwenye hasara yoyote itakayosababishwa na CMO. Je hizi ndio CMO wabunifu wanazihitaji?

**<u>Mapendekezo:</u>**

Sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, inapaswa kurekebishwa na kuelekeza wazi kuwa CMO inapaswa kusajiliwa kama shirika lisilo la kiserikali na lisilotengeneza faida kupitia sheria pendekezi kama **The trustees'Incorporation Act**, **Non Governmental Organization Act** na **Societies Act**. Pia sheria inapaswa kurekebishwa na kueleza wazi kuwa CMO hazipaswi kuendeshwa kwa namna yoyote ile yenye lengo la kutengeneza faida. Pia ieleze wazi kuwa ni marufuku kwa CMO kutumia mirabaha katika kutengeneza faida kwa namna yoyote mahali popote. Sheria hizo tajwa zina uchaguzi wa mara kwa mara kwa hiyo uongozi wa CMO utabadilika kutokana na matakwa ya wanachama (wabunifu)

iv. **Sheria inalinda waarifu dhidi ya makosa ya matumizi mabaya ya ofisi ya umma kwa maslahi binafsi/rushwa kwa kuweka kinga kwa mhusika yoyote kutoka Copyright Office of Tanzania (COOTA).**

Kwa mujibu wa kifungu cha **28** cha sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, kimeongeza kifungu kipya cha **54E** katika Sheria ya Hakimiliki na

Haki Shirikishi iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002).** Katika kifungu hicho cha **54E** kinaagiza kuwa kuwa mjumbe wa bodi ya COOTA au mfanyakazi wa COOTA asishitakiwe kwa jambo lolote atakalofanya kwa **nia njema** katika kutekeleza majukumu yake yaliyoelezwa kwenye sheria hii. Kifungu hiki cha sheria kinaweka mwanya kwa wajumbe wa bodi na wafanyakazi wa COOTA kuhalalisha matumizi mabaya ya ofisi ya umma kwa maslahi binafsi kwa kigezo cha **nia njema**. Kifungu kinapingana na kanuni za maadili ya watumishi wa umma. Tushaona hapo juu sheria ina mapungufu ya kuweka mwanya kwa CMO kutumia vibaya pesa za umma(mirabaha) na huku kifungu hiki kinawalinda wasimamizi wa CMO ambao ni COOTA dhidi ya kushitakiwa na makosa ya matumizi mabaya ya ofisi ya umma kwa maslahi binafsi. Kwa minajiri hiyo sheria imetengeneza mazigira rafiki ya kutekeleza ubadhilifu wa fedha za umma.

**Mapendekezo**

Sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, inapaswa kurekebishwa kwa kufuta kifungu kipya cha **54E** katika Sheria ya Hakimiliki na Haki Shirikishi iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002).** Ili wajumbe wa bodi na wafanyakazi wa COOTA wafanye kazi kwa ufanisi na tahadhari ya hali ya juu. Ni mahakama pekee iachiwe jukumu la kuamua kuhusu **nia njema ya utendaji** wa mjumbe wa bodi au mfanyakazi wa COOTA. Wajumbe wa bodi na wafanyakazi wa COOTA washitakiwe kama watumishi wengine wa serikali wakitenda makosa ya kimaadili ambayo ni jinai.

**v. Sheria imevichagua vifaa vilivyopitwa na wakati katika kulipisha tozo ya vifaa vinavyotumika kubeba, kusambaza, kuhifadhi na kuzalisha kazi za ubunifu.(Copyright Levy on Blank device)**

Kwa mujibu wa kifungu cha **27** cha sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, kimeongeza kifungu kipya cha **48A** katika Sheria ya Hakimiliki na Haki Shirikishi iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002).** Katika kifungu hicho **48A** kimeacha vifaa vyote muhimu vinavyoendana na wakati huu kwenye mabadiliko ya sayansi na teknolojia kama simu, flash disks, kompyuta aina zote, internal na external hard drives nakadharika katika kulipishwa tozo. Badala yake sheria imechagua vifaa ambavyo vipo kwenye hatua ya mwisho ya kuacha kutumika kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Pia sheria haijaelezea mapato yatakayopatikana kutokana na tozo yatagawanywaje.

<u>**Mapendekezo:**</u>

Sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, inapaswa kurekebishwa ili kujumuisha vifaa vyote muhimu vya wakati huu vinavyofaa kulipiwa tozo. Pia kupitia sheria ya bunge sio kanuni, sheria iweke wazi kuwa wabunifu wanapaswa kugaiwa asilimia **85%** ya mapato ya tozo na asilimia 15% itakayobaki itumike

kama gharama za kukusanyia na kugawanya mapato kwa wabunifu. COOTA, na Mfuko wa Sanaa hawapaswi kuhusika kwenye mgao tajwa kwasababu pesa hizo haziwahusu kwa namna yoyote ile. Mapato ya tozo ni mali ya wabunifu yaani fidia yao ya mapato wanayopoteza kupitia vifaa hivyo kwenye uharamia.

vi. **Sheria imeweka adhabu ndogo sana kwa kosa la kuendesha CMO bila leseni.**
Kwa mujibu wa kifungu cha **28** cha sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, kimeongeza kifungu kipya cha **52A** katika Sheria ya Hakimiliki na Haki Shirikishi iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002).** Katika kifungu hicho cha **52A** kifungu chake kidogo **(3)** kinaelekeza kuwa mtu yoyote atakayeendesha shughuli za CMO bila leseni, endapo atatiwa hatiani, atahukumiwa kulipa pesa isiyopungua milioni 10 na isiyozidi milioni 20. Kiasi cha pesa kutumika kama adhabu kunaweza kuwafanya waarifu wasiogope kuendesha CMO bila leseni kwasababu wanaweza kukusanya mirabaha ya kutosha kuwawezesha kulipa adhabu hiyo.

**<u>Mapendekezo:</u>**
Sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, inapaswa kurekebishwa ili kufuta hiyo adhabu na kuweka adhabu mpya ya kurudisha pesa zote walizokusanya, kisha faini ya kiasi cha pesa mara mbili ya walichokusanya na adhabu ya kifungo cha miaka miwili jela. Adhabu zote zitekelezwe kwa pamoja.

vii. **Sheria inaelekeza kuwa rufaa zinazohusu maamuzi ya CMO zitapelekwa Copyright Office of Tanzania (COOTA), ambayo inaweza kuwa sehemu ya mgogoro kwasababu inafanya kazi na CMO.**
Kwa mujibu wa kifungu cha **28** cha sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, kimeongeza kifungu kipya cha **54F** katika Sheria ya Hakimiliki na Haki Shirikishi iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002).** Katika kifungu hicho cha **54F** kifungu kidogo cha **(1)** na **(2)** vinaelekeza kuwa mtu yoyote atakayeumizwa na maamuzi ya CMO atakata rufaa kwenda COOTA, pia mtu atakayeumizwa na maamuzi ya COOTA atakata rufaa kwenda kwa waziri husika.

Ifahamike kuwa CMO wanafanya kazi kwa kusimamiwa na COOTA, hivyo basi COOTA inaweza ikawa sehemu ya mgogoro katika utendaji wa CMO. Ikitokea COOTA wataiagiza CMO kufanya jambo fulani, alafu CMO wakatekeleza kisha likamuumiza mtu mwingine na mtu huyo akaamua kutafuta haki yake, COOTA watahusika kwenye mgogoro huo. Ikitokea hivyo alafu kesi ikapelekwa COOTA, hapo COOTA watakua wanaamua kesi inayowahusu wao wenyewe. Pia migogoro inayoweza kutokea kwenye CMO si vyema kuamuliwa na waziri kwasababu ya masuala mtambuka ya kitaalamu yanayoweza kuibuka.

**Mapendekezo:**

Sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 iliyopitishwa, inapaswa kurekebishwa na kufuta vipengele tajwa kisha kuunda kamati maalumu kupitia sheria ya bunge zenye wataalamu kutoka sehemu mbalimbali kwa ajili ya kusikiliza na kuamua malalamiko ya watu waliumizwa na maamuzi ya CMO au COOTA.

viii. **Sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 na Sheria ya Hakimiliki na Haki Shirikishi iitwayo Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002). Zote zimebeba haki na maslahi ya watu kwenye kanuni ambazo ni rahisi kuzibadilisha endapo atatokea kiongozi asiye mwaminifu.**

Masuala ya Mirabaha, Masuala ya CMO, Masuala ya mfuko wa sanaa na Masuala ya Tozo za Hakimiliki yamebeba haki za wabunifu nchini, hivyo basi hayapaswi kuendelea kuwekwa kwenye kanuni ambazo zinaweza kubadilishwa na maamuzi ya mtu mmoja.

**Mapendekezo:**

Sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 na Sheria ya Hakimiliki na Haki Shirikishi iitwayo Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002). Sheria hizo zinapaswa kufanyiwa marekebisho ili kuingiza haki za wabunifu kwenye sheria zilizotungwa na bunge ambazo ni ngumu kuzibadilisha bila kuhusisha serikali nzima na wananchi. Hii itasaidia kulinda haki za wabunifu kizazi hadi kizazi. Masuala ya Mirabaha, Masuala ya CMO, Masuala ya mfuko wa sanaa na Masuala ya Tozo za Hakimiliki yamebeba haki za wabunifu

## B. HITIMISHO:

Utaratibu wa kutunga sheria kwa mujibu wa kanuni za bunge unaelekeza kuwa mchakato mzima wa kutunga sheria lazima upitie hatua ya ushirikishaji wa wadau husika ambao sheria hiyo itawahusu. Hivi karibuni tumeshuhudia sheria ya hakimiliki na Hakishirikishi, namba 7 ya mwaka 1999 ikifanyiwa marekebisho bila kushirkisha wadau. Hali hiyo husababisha utungwaji wa sheria zisizo na msaada kwa wananchi. Tunaisihi na kuiomba serikali kufanya marekebisho ya **Sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022** na **Sheria ya hakimiliki na Hakishirikishi, namba 7 ya mwaka 1999** kwa kushirikisha wadau ili kuondoa mapungufu mengi yaliyopo zaidi ya haya yaliyoorodheshwa.**Mfano: Uhuru wa kujieleza kwenye kazi za kibunifu, Usawa wa kijinsia kwenye shughuli za sanaa na utamaduni, kukosa uwazi kwenye soko la kazi za sanaa na utamaduni, sheria kupitwa na wakati nakadharika**

**ASANTENI**

(Kazi iendelee)

**Wako katika kujenga Taifa**

**Mkurugenzi Mkuu wa Utawala**

**WAKILI JOSHUA MSAMBILA**